

SWALI: Mwandishi wa kitabu cha Wafalme alikuwa nani?

---

Biblia haijaweka bayana aliyekuwa mwandishi wa kitabu hiki, lakini kufuatana na hadithi za kiyahudi huaminika kuwa nabii Yeremia ndiye alikuwa mwandishi wa vitabu hivi viwili vya wafalme.

Kitabu hichi kinaeleza kwa kina tawala za kifalme Kuanzia Mfalme Sulemani, na kugawanyika kwa taifa la Israeli pande mbili, hadi kuanguka kabisa kwa taifa lote la Israeli kwa kuchukuliwa utumwani Ashuru na Babeli. Miongoni mwa Wafalme wapo waliosimama vema, lakini pia wapo wengi waliolikosesha taifa la Israeli, Wa kwanza alikuwa ni Yeroboamu ambaye ndiye aliyeupokea ufalme uliogawanyika yeye aliunda sanamu na kuzisimamisha kaskazini na kusini mwa Israeli, ili waisraeli wakamwabudu Mungu huko. Machukizo ambayo yaliendelea hivyo kwa muda mrefu, ijapokuwa zilikuja kuondolewa hizo sanamu na mfalme aliyeitwa Yosia, lakini bado hasira ya Mungu haikupoa kwa mambo mengi mabaya waliyokuwa wanayatenda wana wa Israeli, Hadi walipofikia hatua ya kuhamishwa.

Kwa urefu wa uchambuzi wa vitabu hivi waweza fungua hapa upate kujisomea >>> VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 5

Bwana akubariki.

Je! Wewe umepokea wokovu wa Roho yako kwa Kristo Yesu? Kama ni la!  
Basi wakati ndio huu wa kufanya geuko la dhati, moyoni mwako. Ikiwa  
upo tayari basi fungua hapa kwa mwongozo huo>>> KUONGOZWA SALA  
YA TOBA

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako  
bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge  
na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

## WAFALME WALIOTAWALA ISRAELI.

Mwandishi wa kitabu cha Filemoni ni nani?

Mwandishi wa kitabu cha Zaburi ni nani?(Opens in a new browser tab)

Sala ya baraka (Hesabu 6:24-26).(Opens in a new browser tab)

Rudi Nyumbani

Share on:  
WhatsApp